KUSOMA ACTIVITIES GREDI 1

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (Alama 5)

Sikiliza kwa makini nikikusomea kifungu hiki kisha ujibu maswali nitakayokuuliza.

Wiki moja ina siku saba. Siku ya kwanza ni Jumamosi. Mimi huenda kanisani siku ya Jumapili. Jumatatu, Jumanne, Jumatano, Alhamisi hadi Ijumaa ni siku za kuenda shuleni. Mimi hupumzika siku ya Jumamosi na kufanya usafi.

a. Siku ya kupumzika ni gani?
b. Siku ya kufanya usafi ni gani?
c. Wiki moja ina siku ngapi?
d. Siku za kuenda shule ni ngapi?
e. Siku ya kwanza ya wiki ni gani?

2. **KUSOMA KWA SAUTI**

   Soma kifungu hiki kwa sauti.

   Ni vyema watoto kuwa na heshima kwa wakubwa wao. Iwapo mtoto amemkosea mwenzake amwambie pole. Akipewa kitu aseme asante.
   Pia mtoto anapotaka kitu ama kuomba ruhusa atumie maneno kama tafadhali ama nisaidie. Pia ni vizuri kuomba msamaha unapomkosea mwenzako.'